



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA  
THE HANSARD**

Tuesday, 24<sup>th</sup> June, 2025

Third Assembly – Fourth Session  
THIRTY SECOND SITTING

*[The County Assembly met at 11:09a.m at the County Assembly Buildings]  
[The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir) in the Chair]*

**PRAYERS**

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): You may take your seats.  
Yes, Clerk?

**COMMUNICATION FROM THE CHAIR**

STUDY VISIT FROM MAGONGO HIGH VISION JUNIOR SCHOOL

Honourable Members, I wish to bring to you the attention of this Honourable House that we have students and teachers from Magongo High Vision Junior School. I recognize the presence of the Members which consist of;

1. Michelle Kitota
2. Mariana Wayua
3. David Nyale
4. Karen Michelle
5. Dennis Mutua
6. Francis Kahiga
7. Noria Aftin
8. Suleiman Ali
9. Stacy Mueni
10. Dorcas Khaemba
11. Lois Kyalo
12. Joseph Salim
13. Richard Waweru
14. Emmanuel Omondi
15. Gift Kabia
16. Genevieve Whitney
17. Sherley Oduor
18. Victoria Adhiambo

19. Violence Marina
20. Elijah Kyalo
21. Harmony Mutharimi
22. Alvin Mwakuro
23. Scarlett Angelene
24. Nora Mgendi
25. Mr. Suleiman Jack
26. Mr. Collins Otieno

On behalf of the County Assembly, I welcome you to the County Assembly of Mombasa.  
*Karibuni sana. Yes, Clerk?*

### ADJOURNMENT OF THE COUNTY ASSEMBLY

Yes, Honourable Athman Mwamwiri. Please move the Motion.

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, naomba kuleta hoja ya kuahirishia vikao vya Bunge. Kwa mujibu wa kanda zetu za kudumu Mheshimiwa Spika hoja ya nidhamu 30 sehemu ndogo ya kwanza Bunge hili linaombwa kuahirisha vikao vyake hadi tarehe moja siku ya Jumanne tarehe moja mwezi wa saba mwaka wa 2025 nimuombe Mheshimiwa Kiranja wa Walio Wengi katika Bunge hili Mheshimiwa Prischilla kuweza kuunga mkono hoja hii.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Prischilla.

**The Chief Whip** (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Members, I now propose the question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on Adjournment of the County Assembly be considered by this Honourable House in the same terms as moved?

*[Question proposed and agreed to]*

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, please make your contribution to the Motion.

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika hoja hii sidhani kama itakuwa na mjadala mkubwa kwa sababu kwa mujibu wa katiba yetu, moja wapo ya majukumu tuliopewa ni usimamizi wa utawala wa serikali hii. Mheshimiwa Spika tunapo ongea kuna zoezi ambalo katika kata zetu limekusudiwa kuendelea zoezi la kuweza kupeana fomu za basari kwa wanafunzi ama wazazi walio wanafunzi katika shule za bweni na ni jukumu letu sisi kuhakikisha kwamba zoezi hili limetendeka pasipo na ubaguzi, upendeleo, wala unyanyasaji kwa wazazi wetu. Mheshimiwa Spika hivyo basi hii ni moja wapo ya sababu ya kwamba kikao hiki kiweze kuahirishwa ili wawakilishi waweze kurudi nyanjani kusimamia zoezi hili lakini pia tunayo taarifa na walishi rasmi ya kwamba kiongozi wa chama chetu chama kilicho na Waheshimiwa wengi toka Bunge hili Mheshimiwa ambaye ni waziri mkuu wa taifa hili Mheshimiwa Raila Amolo Odinga atawasili rasmi katika majira ya saa nane katika uwanja wetu wa ndege wa kimataifa wa Moi na ni jukumu letu Mheshimiwa sisi ambao tumelelewa na kukulia katika chama hiki kuweza kumkaribisha rasmi na kuungana ne katika ziara yake ya mji wetu huu wa pwani wakianzia hapa Mombasa. Kwa hivyo si ni dhamu Mheshimiwa Spika sisi kama watoto wa chama kubakia katika kikao wakati Mheshimiwa kiongozi wa chama yuko nasi hapa na amekuja kwa misingi ya kimaendeleo ikiwemo kufungua shule ya chekechea ya kule

Maganda Mheshimiwa Spika hivyo naomba Waheshimiwa wenza tuweze kuwajibika katika hili turudi nyanjani kupeana fomu za basari na majira ya saa nane kuungana na kiongozi wetu wa chama Mheshimiwa Raila Amolo Odinga. Ahsante Mheshimiwa Spika naomba Waheshimiwa waweze kuunga mkono hoja hii.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Juma Kambi?

**Hon. Juma Mwalimu:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kuunga mkono hoja hii iliyoletwa na kiongozi wa wengi Bungeni kwa sababu ya zile sababu walizozitoa. Kwanza ni ugawi wa fomu zetu za basari na vile vile kiongozi wa chama chetu cha ODM Mheshimiwa baba Raila Amolo Odinga uwaja hapa. Kwa hio, sisi kama jeshi lake kama wafuasi wake wa dhati hatuna budi kuenda kumuunga mkono. Kwa hivyo ni haki yetu kufunga hili Bunge kidogo kwa huu wakati uliobaki ili tuweze kufanya hizi shughuli mbili tatu kwa manufaa ya watu wa Mombasa. Mimi nitasema ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kupata fursa hii. Ahsante sana.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Manuari Seif.

**Hon. Juma Manuari:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi pia nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Pili, nimuunge mkono ndugu yangu kiongozi wa wengi katika Bunge la Mombasa. Mheshimiwa Spika leo ni siku tamu sana na ni siku nzuri sana kwa sababu pia tumetembelewa na watoto wetu pale wadogo niwaambie watoto karibuni sana hapa ndiyo Bunge la Mombasa na mkitoka hapa mkirudi nyumbani muwaambie wazazi wenu nyinyi pia leo mumekea wa Bunge na mumeingia ndani ya Bunge na mtakua Wabunge. Si ndiyo hivyo? Na Mheshimiwa Spika nichukue nafasi hii pia kumpa pongezi kiongozi wetu wa Kiranja wa Wengi katika Bunge la Mombasa dada yetu Prischilla Mumba kwa zile nywele zilivyo vizuri na pia niwaambie Waheshimiwa wengine hebu waige mfano wake maana amekaa kama Malkia Elizabeth. Kwa hayo mengi machache ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Wainaina?

**Hon. Ngugi:** Ahsante Mheshimiwa Spika mimi pia nimesimama kuunga mkono hoja. Asante Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Pamela?

**Hon. Ojala:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity also to contribute my views. Mr. Speaker, before I proceed, I want to thank the Almighty God for having given us this golden opportunity to see the day of today. Also to acknowledge the presence of students from Magongo High Vision Junior School you are highly welcome, feel at home this is a House of debate and record in future we also wish you will also become one of us you feel at home. Mr. Speaker, when I am embarking on the discussion I stand to support the Motion Adjournment of the County Assembly. I want also Mr. Speaker to congratulate our leader of majority, Athman Mwamwiri, for the important Motion before us Mr. Speaker. Mr. Speaker us as honorable members, Mr. Speaker, today we have two important occasions at our County One is the issuance of the bursary Mr. Speaker as you know this exercise is very critical and as Honourable Members, we must be at our Ward level to witness the exercise for the accountability Mr. Speaker. Secondly, as the majority mention has mentioned Mr. Speaker today, we have an important man coming to our County the party leader is Excellency Right Honourable Amolo

Odinga. He is the father of the nation Mr. Speaker and it will be very bad as the sons and sisters of Raila to be in the parliament continuing with the debating while our Party leader is around Mr. Speaker I support the adjournment of the County Assembly Mr. Speaker. Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you any other Member wishing to contribute? Yes, Honourable O.J?

**Hon. Ong'au:** May I also take this opportunity Mr. Speaker to support the Motion and may I also take this opportunity also to welcome the students from *Magongo* and their priest who is also a member of this County Assembly Mheshimiwa Madialo. Thank you, I support.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Honourable Madialo while you are seated at the gallery may I advise you that it is not permissible to wear the cap that you are wearing. Please, be advised. Yes, Leader of Majority, please respond to the Motion.

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Nimeshukuru Waheshimiwa wenza kwa kuweza kuchangia na kuunga mkono hoja hii lakini pia ni watake radhi wanafunzi wetu ambao tuko nao hapa siku ya leo walitarajia labda tungekua na hoja ndefu lakini kwa sababu za kimsingi wamekuja wakati ambao tunaahirisha kikao lakini yale mengine ambayo wangetaka kujifunza Mheshimiwa Spika Bunge liko wazi wanaweza rudi siku nyengine lakini pia leo tuna wafanyi kazi waliobobea katika Bunge hili wanaweza kuhoji na kuuliza maswali kuweza kuelekezwa na angalau kupata elimu walio kusudia katika msafara wao huu isiwe wamekuja bila natija ya msafara wao Mheshimiwa Spika. Kwa hayo Mheshimiwa Spika nashukuru Waheshimiwa turudi nyanjani tuwakilisha hili na tukutane maganda tukimkaribisha baba na zoezi la ufunguzi wa shule yetu ya chekechea. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you Members for your contribution to this Motion. I now put the question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on Adjournment of the County Assembly be approved by this Honorable House in the same terms as debated?

*[Question put and agreed to]*

Honourable Members, the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on Adjournment of the County Assembly is adopted by the House. Yes, Clerk?

### ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Tuesday 1<sup>st</sup> July, 2025 at 10:00a.m. Thank you.

The House rose at 11:24a.m.